Ukurasa wa dokezo

Watu wenye ulemavu na hatua za ulinzi na usalama

Ukurasa huu wa dokezo unaelezea kanuni kuu ambazo zinapaswa kuzingatiwa wakati wa kutekeleza mbinu za ulinzi na kutumia rasilimali kwenye kituo cha rasilimali na Usaidizi. Pia una mapendekezo maalum.

Kanuni 1:

Kujumuishwa na kutobaguliwa

Kutowahukumu watu wenye ulemavu katika juhudi za kuwakinga, kuwazuia, kutoa habari na kufanya kuongezeka kwa hatari dhidi yao ya kunyanyaswa kijinsia, kudhulumiwa na kushambuliwa (SEAH). Watu wenye ulemavu mara nyingi, bila kufahamu, hutengwa kutoka kwa shughuli za ulinzi, hali ambayo humaanisha kwamba hatari maalum wanazopata hazijumuishwi katika michakato ya kwanza ya mipango.

Kwa hivyo:

- Hakikisha unawazingatia watu wenye ulemavu kwenye michakato yote ya mipango ili kuhakikisha kwamba ulinzi wa pamoja 'inawekewa mikakati' tangu mwanzo
- Fanya kazi kwa kushirikiana na watu wenye ulemavu wa kila umri, jinsia na hali ya kiuchumi – jamii na mashirika yao ya uwakilishi kama wadau muhimu katika programu.
- Zingatia kuwa na aina mbali mbali ya wafanyakazi ili kuongeza uwezo wa watu mbalimbali kukuwa pamoja (kwa mfano, wanawake wa asili ya wenye ulemavu).

---

[1] Hizi zinaambatana na kanuni za UNCRPD; yaani: Heshima ya utu asili, uhuru wa mtu binafsi ikiwa ni pamoja na uhuru wa kufanya maamuzi mwenyewe, na uhuru wa watu; Kutobaguliwa; Ushiriki kamili na yenye ufanisi na ujumuishwaji katika jamii;

Heshima ya utofauti na kuwakubali watu wenye ulemavu kama sehemu ya utofauti wa wanadamu na ubinadamu; Usawa wa fursa; Upatikanaji; Usawa kati ya wanaume na wanawake; Heshima ya uwezo unaobadilika wa watoto wenye ulemavu na heshima ya haki ya watoto wenye ulemavu kuhifadhi utambulisho wao.

- Tengeneza orodha za ukaguzi ambazo zinaonyesha njia za kuwaleta watu mbalimbali pamoja (kwa mfano, kuhakikisha kuwa orodha hiyo inaonyesha mahitaji tofauti ya wanawake wote walio na shida ya kuona na wale walio na shida ya kusikia - njia za mawasiliano zitatofautiana).
- Wakati wa kuandaa warsha au semina yoyote au mafunzo, hakikisha kwamba eneo, vifaa na mbinu ya uwezeshaji zinazingatia maswala ya jinsia na ulemavu, ni jumuishi na zinafikia watu wote.

Upatikanaji

Huduma zisizoweza kupatikana zinaweza kuongeza hatari. Watu wenye ulemavu wanaweza kuwa na ugumu wa kupata huduma kwa njia sawa na watu wasio na ulemavu. Hii inaweza kuwaweka katika hali zilizo na hatari kubwa, kama vile usafi wa mazingira, kwa mfano. Huduma za kusaidia watu waliopitia SEAH pia zinaweza kuwatenga watu wenye ulemavu bila kujua, ikiwa huduma hizo zinatolewa katika miundo ambayo haipatikani au ikiwa wafanyakazi hawana uelewa kuhusu ulemavu.

Njia za mawasiliano zisizo jumuishi zinatenga watu kwa hivyo zina ufanisi mdogo. Mtu ambaye ni kipofu au aliye na ugumu wa mawasiliano na kusoma pia anaweza kupata changamoto katika kufanya malalamiko, haswa ikiwa kuna utaratibu wa kuripoti ambao unahitaji mtu kuandika. Vivyo hivyo, njia mbadala za kuripoti, kwa mfano kwa viziwi, au watu wenye ulemavu wa akili unaweza kuathiri usiri na usalama wa mtu - na hivyo kuongeza hatari zaidi.

Kwa hivyo:

- Zingatia ongezeko la hatari zinazoweza kusababishwa na kukosa upatikinaji wakati wa kubuni na kutekeleza mradi
- Hakikisha kuwa kuna utaratibu zaidi ya mmoja wa kuripoti au kutoa taarifa; na kwamba zimebuniwa kwa kushirikiana na watu walio na ulemavu mbalimbali ambao watahusika katika mpango huo.

Habari zinazoweza kupatikana na zilizojumuishi zikitolewa kwa njia mbali mbali huongeza ufikiaji wa ujumbe. Watu lazima wawezeshwe kuelewa haki zao kwa njia inayowafaa, kwamba hawalazimiki kubadilishana ngono kwa bidhaa au huduma; au kwamba wana haki ya kupata huduma sawa na mtu asiye na ulemavu. Vile vile wafanyakazi wa shirika za misaada au maendeleo ya watu wenye ulemavu wanahitaji kujihisi salama ndani ya mazingira yao ya kazi na kuona ishara wazi kutoka kwa shirika kwamba unyanyasaji wa kijinsia (na aina zingine za vitendo vya kibaguzi) haukubaliki. Lazima pia wajue mahali pa kupeleka ripoti na pa kupata huduma wanazohitaji.

Kutoa taarifa au habari na kuongeza uelewa unaotekelezwa na mashirika ya misaada unapaswa kuzingatia mahitaji ya idadi ya watu na kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu (ambao hawawezi kuwa na ufikiaji sawa wa elimu au ambao hawawezi kuona, kusikia au kuwasiliana) pia wanapokea habari wazi au sahihi.

Kwa hivyo:

- Zingatia kuwashirikisha watu wenye ulemavu na mashirika yao wakilishi katika kubuni ujumbe wa SEAH na mawasiliano ili kuhakikisha kuwa huduma mbali mbali zinajumuishwa
- Shirikisha watu wenye ulemavu tangu awali katika shughuli za kutoa taarifa na uelimishaji ili kuhakikisha kwamba ujumbe ni sahihi, unafaa na kukubalika

Usawa wa kijinsia

Wanawake, wasichana na vijana walio na ulemavu wako katika hatari kubwa ya SEAH kwa sababu ukosefu wa usawa wa kijinsia huambatana na ubaguzi wa walemavu. Watu ambao wanatafuta fursa za kuwanyanyasa wanawake, wasichana na vijana wanaweza kulenga wale wenye ulemavu, kwa sababu wanaweza kudhani kuwa wao ni walengwa wanyonge,ambao pia hawataweza kulalamika, au kuaminiwa ikiwa watalalamika, kwa sababu mbali mbali zilizotajwa hapo juu. Watu wenye ulemavu na mashirika yanayowawakilisha pia huenda hayana uelewa mkubwa juu ya maswala fulani yanayowapata wanachama wao wanawake; na huenda wanawake hawako katika nafasi za uongozi hali ambayo huongeza tena ukosefu wao wa sauti.

Kwa hivyo:

- Unaposhirikiana na watu wenye ulemavu na mashirika yao wakilishi, tafuta uwakilishi mbali mbali ambao unawajumuisha wanawake, wasichana na vijana walio na ulemavu kutoka mipangilio tofauti na watu walio na ulemavu tofauti
- Zingatia maswala ya ulemavu katika shughuli zote za ujumuishaji wa kijinsia na usawa wa jinsia ambazo zina lengo la kuwezesha wanawake, wasichana na vijana wenye ulemavu.

Vidokezo vikuu vya kujumuisha ulemavu kwenye ulinzi na usalama

Juhudi za Ulinzi zina hatua nne. Kila hatua inauliza swali kwa mashirika kutafakari, hatua wanazochukua za kuimarisha sera zao za ulinzi, pamoja na mazoea na tamaduni zao za kuzuia na kukabiliana na SEAH:

- Ulinzi na usalama ni nini?
- Jinsi ya kutathmini na kupanga ulinzi na usalama
- Ni nini kinachohitajika kuhakikisha kuna ulinzi na usalama?
- Nini cha kufanya ikiwa kuna tatizo

Vidokezo vikuu vilivyo orodheshwa kwenye jedwali iliyopo hapa chini sio kamili lakini vinafaa kwa hali zote.

Upatikanaji	Uwezo	Iliyolengwa

Fanya kazi na watu wenye ulemavu na mashirika yao wakilishi kukagua jinsi programu inawashughulikia walemavu, na jinsi inavyotoa taarifa, habari, mawasiliano na miundo mbinu.	**Boresha ujuzi na uelewa wa ulemavu kati ya wafanyakazi, washirika na wadau wengine (pamoja na watoa huduma ya kisaikolojia, polisi, watoa huduma kwenye vituo vya afya na wafanyakazi wa elimu). Ikiwezekana, shirikisha watu wenye ulemavu kama wakufunzi, ili waweze kukabiliana na kanuni mbaya za jamii na ukosefu wa usawa wa nguvu ili kuzuia SEAH**	**Tambua mitandao inayohusika katika malalamiko na uchunguzi wa SEAH ambayo inaweza kusaidia watu wenye ulemavu (haswa wale walio na mahitaji ya juu ya msaada) wanaohusika na malalamiko na uchunguzi.**
Hakikisha taarifa ya SEAH na njia za kuripoti au kutoa taarifa zinapatikana kwa miundo mbalimbali na kusambazwa kwa njia tofauti (redio, kupitia viongozi wa jamii, na njia yasio ya fasihi nk.)	**Himiza uajiri wa watu wenye ulemavu na wanawake ili kubadili mitazamo na kuwakilisha watu wa jinsia maalum na maswala ya ulemavu katika muundo na utekelezaji wa mradi.**	**Lenga haswa wafanyakazi ambao wanachukua muda mrefu bila kusimamiwa wakati wana kushughulikia wanawake, watoto na watu wenye ulemavu ili kuwapamsaada, mawaidha na mafunzo kuhusu ulinzi na usalama**
Hakikisha vifaa na miundo mbinu ya mazingira hauweki watu wenye ulemavu katika hatari zaidi (vifaa vya usafi wa mazingira na vyoo wanavyotumia vinapaswa kuwa nakufuli)	**Fanya kazi na wanawake na wanaume wa kila umri na vikundi vya walemavu kubuni njia mbalimbali za faragha ili kutoa taarifa ambazo zinaonyesha mahitaji ya watu walio na matatizo tofauti (k.m. watu ambao ni viziwi-vipofu / wenye shida nyingi) ili kuhakikisha usiri**	**Fanya kazi na watu wenye ulemavu na mashirika yao ya wakilishi pamoja na vyama vya wazazi kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanajua haki zao, majukumu, michakato ya kuripoti na kuimarisha njia za ndani za SEAH.**
Weka taratibu na mifumo za kupata maoni ya watu walio na ulemavu kwenye mpango wowote wa ulinzi na usalama ili kuangalia kiwango ambacho ujumuishaji wa walemavu umefikiwa		